GOVERNMENT NOTICE No. 720 published on. 6/2023

SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA,
(SURA YA 191)

# KANUNI

*(Zimetengezwa chini ya kanuni ya 230(2)(f))*

MAREKEBISHO YA KANUNI ZA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (MARUFUKU YA MATUMIZI YA VIFUNGASHIO VYA PLASTIKI NA LAKIRI ZA CHUPA) ZA MWAKA 2023

Jina

TS.Na. 394 la 2019.

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Usimamizi wa Mazingira Marufuku ya Matumizi ya Vifungashio vya Plastiki na lakiri za Chupa za Mwaka 2023. na zitasomwa pamoja na Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Marufuku ya Matumizi ya Vifungashio vya Plastiki na lakiri za Chupa) za Mwaka 2019, inayorejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 32

2. Kanuni kuu inarekebishwa katika kanuni ya 32 kwa-

(a) kufanya maudhi ya kanuni ya 32 kuwa maudhui ya kanuni ya 32(1);
(b) kuongeza kanuni ndogo ya (2), (3) na (4) mara baada ya kanuni ndogo ya (1):

"(2) Rufaa chini ya kanuni ndogo ya (1) itawasilishwa kwa njia ya barua ikieleza, sababu za rufaa ikiambatishwa na maamuzi ya Baraza na nyaraka zingine muhimu Waziri atakazohitaji baada ya kupokea rufaa hiyo.

(3) Waziri atatakiwa kutoa maamuzi ya rufaa hiyo ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya kupokelewa rufaa hiyo.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (3), Waziri atatakiwa kumjulisha mwomba rufaa maamuzi ya rufaa na sababu za maamuzi hayo ndani ya siku saba".

Dodoma,
21 Septemba, 2023

SELEMANI SAIDI JAFO,
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makam wa Rais (Muungano na Mazingira*